Je, unajua kwamba...?

Leo hii, asilimia 50 ya idadi ya watanzania ni watoto. Wengi wa watoto hao huishi mazingira magumu na hatarishi: badhi yao hukumbwa na **unyanyasaji** au **kutelekezwa** katika familia zao, badhi yao huvumilia **ulevi** wa wazazi au walezi wao pamoja na **ugomvi** majumbani mwao, badhi yao inawabidi wajisaidie wao wenyewe au familia zao kifedha, na wengine wamejikuta wanaishi katika **mazingira hatarishi mitaani**. Hivi sasa, katika jamii yako, wapo watoto ambao wanakosa mahusiano mazuri na mtu mzima ambaye anawajali. Matokeo yake kwa watoto ni kutoroka shuleni, kushindwa kuendeleza maadili mazuri au kujihusisha katika matendo hatarishi. Badhi yao wanaamua kwenda kuishi mitaani.

WEWE unaweza kusaidia kuzuia matokeo haya. Watoto wanahitaji mfano mzuri kutoka kwa watu wazima ambao huwa mfano wa kuigwa unaotoa **ushauri**, **urafiki** na **hali ya kujali**. Mkombozi inaamini kwamba kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya kuwasaidia watoto wetu kinapatikana katika jamii yetu. Kama mwanajamii, ni rahisi kwako kumwezesha mtoto kuchagua mwelekeo sahihi katika maisha...

Kujenga uwezo wa watoto.
Kushirikisha familia.
Kuwezesha jamii.

Mkombozi

Kujenga uwezo. Kushirikisha. Kuwezesha.

Tumia muda MFUPI
Toa matokeo MAKUBWA

Kuwa Kaka Mkubwa / Dada Mkubwa

S.L.P. Box 9601
Moshi, Tanzania

Moshi: +255 27 2754793
Arusha: +255 27 2544319

info@mkombozi.org
www.mkombozi.org



Mkombozi

Kaka Mkubwa / Dada Mkubwa ni nini? KM/DM ni mpango ambao inaboresha maisha ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu/hatarishi kwa kutumia mahusiano mazuri na wanajamii wa Moshi na Arusha mjini ambao wako tayari kujitolea...

www.mkombozi.org

Tumia muda MFUPI. Toa matokeo MAKUBWA.

Unataka kujua zaidi kuhusu KM/DM?

Tutembelee: Unakaribishwa kutembelea ofisi yetu ya Arusha - tuko maeneo ya Kaloleni, nyuma ya hoteli ya Golden Rose. Pia, unakaribishwa kutembelea ofisi yetu ya Moshi - tuko maeneo ya Majengo, karibu na makampuni ya Motex na Rajinder Motors.

Kwa mawasiliano zaidi: Wasiliana na anayehusika na mpango huu wa KM/DM - Amani Lucas - kwa kutumia simu au barua pepe: 076 788 1175 / amanilucas@mkombozi.org

Fikiri ZAIDI. Tenda ZAIDI. Watoto ambao wanapata muda wa kuwa na Kaka au Dada Mkubwa huendeleza uwezo wao wa kujiamini, kujifunza jinsi ya kufanya maamuzi sahihi, kujijengea uwezo wa kujitegemea na kuyapa mafunzo kipaumbele zaidi. Watoto wanaopata usimamizi wa watu wazima hujiepusha na tabia mbaya au hatarishi na hufanya vyema katika masomo yao shuleni. Kuwa Kaka au Dada Mkubwa inamaanisha kufanya kitu cha muhimu. Wewe ukiboresha maisha ya mtoto, maisha yako pia yataboreka na kuwa na maana zaidi kwako binafsi.

Wewe mwenye nia na moyo wa kusaidia

unakaribishwa!

Je, unapenda watoto wawe na furaha? Je, unapenda kujitolea kusaidia jamii yako? Je, uko tayari kutumia muda wako mfupi kuwa pamoja na mtoto? Je, wewe ni msikilizaji mzuri? Je, unaweza kutegemewa? Je, umri wako ni zaidi ya miaka 19?

Kama ndio, wewe una sifa zinazohitajika kuwa Kaka au Dada Mkubwa! Huhitaji ujuzi maalum au pesa - unahitaji tu kuwa na moyo ambao unajali kuwasaidia watoto kujiendeleza.

Mkombozi ni mojawapo ya asasi za kiraia ambayo inajihusisha na maswala ya watoto kaskazini mwa Tanzania. Kwa mwaka, inafanya kazi na watoto na familia zaidi ya 1000 katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Dira ya Mkombozi ni kusaidia watoto na vijana kukua kiakili, kimwili na kiroho na kujenga jamii inayojali zaidi kwa watu wote, ambamo mshikamano umejengwa na kufuata msingi na utawala wa sheria. Tunatenda kama kichocheo kwa ajili ya maendeleo kwa ujumla.

Ndoto ya Mkombozi ni ulimwengu ambamo watoto wote na vijana wanapewa kipaumbele na wanaweza kupata fursa zitakazowasaidia kuwa watu waliokamilika, wasaidizi na nguvukazi kwa taifa kwa ajili ya jamii iliyo na usawa na ya kidemokrasia zaidi. Tunaamini kwamba tunaweza kuboresha haki za kijamii kwa njia ya ushirikishwaji na kufanya kazi kwa mshikamano.

Nini kinatarajiwa kutoka kwangu kama Kaka / Dada Mkubwa?

Unakubali kujitolea kuwa Kaka / Dada Mkubwa kwa ajili ya mtoto utakayepangiwa na Mkombozi kwa muda wa mwaka mzima.

Unakutana na Kaka au Dada wako Mdogo angalao kwa muda wa saa moja kila wiki.

Unakuja kwenye mikutano na mafunzo ya Mkombozi mara nne kwa mwaka.

HUTAKIWI kumpa huyo mtoto vitu au pesa yo yote.

HUTALIPWA malipo yo yote na Mkombozi.

Mimi ninapata nini nikiwa Kaka / Dada Mkubwa?

Uzoefu na maarifa/ujuzi.

Mafunzo ya msingi katika kujenga mahusiano na watoto, maendeleo ya watoto pamoja na unyanyasaji na ulinzi wa watoto.

Roho ya kujitolea katika kuwasaidia wengine.

Uzoefu katika kusaidia na kujali watoto walioko kwenye mazingira magumu.

Kujitambua na kuwajibika katika jamii yako.

Baada ya kujitolea kwa muda wa mwaka mmoja, Mkombozi itatambua/itaheshimu jitihada zako kwa kukupa cheti cha kuthamini mchango wako.

Nitumie mchakato gani nikitaka kuwa Kaka / Dada Mkubwa?

1. Uwasiliane na Mkombozi ili upate fomu ya maombi.
2. Ututumie fomu yako pamoja na majina ya wadhamini wawili.
3. Utafanyiwa interview (usaili) na anayehusika na mpango wa Kaka/Dada Mkubwa.
4. Umkaribishe anayehusika kukutembelea nyumbani kwako kuongea na familia yako na majirani zako.
5. Mkombozi itakujulisha kwamba umekubalika kuwa Kaka / Dada Mkubwa.
6. Uje kwenye kikao cha utambulisho.
7. Mkombozi itakuunganisha na mtoto.